

Bibilia ya watoto

Inaleta



Mtu atumwa
kutoka kwa
Mungu



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus
Alastair Paterson

Imerekebishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.,

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii,lakini bila ya kuuza.



Siku moja ndani nya hekalu ya Mungu, kuhani mzee aliyeitwa Zakaria alikuwa akitoa sadaka. Nje, watu walikuwa wakiomba. Mara tu, Zakaria akaanza kutetemeka.



Malaika alikuwa amekuja. "Usiogope," akamwambia.
"Mungu amenitura. Mke wako atapata mwana.

Mtamwita Yohana. Yeye atajawa na
Roho Mtakatifu kutoka kuzaliwa kwake.
Yeye ataweleta wengi kwa
Bwana."



"Zungumza nasi Zakaria." Watu waliokuwa
nje wakasema. Hawakujuu kuwa
malaika Gabrieli alisema kuwa Zakaria
hangeweza kuzungumza hadi
mtoto yule atakapozaliwa
kwasababu hakuamini neno lile
kutoka kwa Mungu. Alidhani
kuwa mke wake
alikuwa mzee



sana kuzaa
mtoto.

Nyumbani, Zakaria akaandika
yote aliyoambiwa na malaika.
Elisabeti, mke wake
akastaajabu. Walikuwa
wameomba kupata mtoto.
Je, ingefanyika sasa?





Baada ya muda
mfupi Elisabeti
akajua kuwa
angezaa mtoto.
Hapo akamsifu
Mungu. Siku
moja jamaa
yake, Maria
akamtembelea.
Maria pia
alikuwa
akitarajia
kuzaa mtoto.



Maria alipofika, Elisabeti akamhisi mtoto akiruka kwa shangwe ndani ya tumbo yake. Elisabeti akajazwa na Roho Mtakatifu. Alijua mtoto wa Maria angekuwa Bwana Yesu Kristo. Pamoja wanawake wale wawili wakamsifu Mungu kwa furaha.



Mwana wake Elisabeti akazaliwa kama vile Mungu aliahidi. "Mwite Zakaria kama babake," kuhani wengine walisema. Zakaria akakumbuka Mungu alivyosema. "La! Jina la mtoto ni Yohana." Wakati Zakaria alimaliza kuandika maneno haya, kinywa chake kikafunguliwa na akaweza kuzungumza tena. Halafu akamsifu Mungu.



Yohana alipokuwa mkubwa akawa kama Eliya, mtumishi mkuu wa Mungu.



Yohana aliwahubiria watu akiwaelezea kuwa Mwana wa Mungu anakuja hivi karibuni kuwabariki. Viongozi wayahudi hawakumpenda Yohana kwasab-abu aliwaambia, "Mtubu! Acheni kutenda dhambi." Hawakutaka kusikia kuhusu dhambi zao.



Watu wengine walimwita Yohana Mbatizaji
kwasababu aliwatumbukiza watu ndani ya maji
kuonyesha kuwa walitubu dhambi zao.

Siku moja Yesu akamjia Yohana
ili ambatize. "Wewe
ndiwe unatakikana
kunibatiza," Yohana
akasema. Lakini Yesu
akamwambia,
"Na itendeke."
Na Yohana
akambatiza.



Baada ya ubatizo wa Yesu, Yohana akaona Roho Mtakatifu akimshukia Yesu kwa mfano wa kiwiliwili. Hii ilikuwa ishara kutoka kwa Mungu. Yohana alijua kuwa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Yohana alimwita Yesu Mwana Kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya dunia.



Yohana aliwaleta wengi kwa Mungu. Lakini Herode, mfalme mwovu, alimfunga Yohana gerezani. "Ni

dhambi kwako
kumchukua Herodia,
mke wa ndugu yako
kama mke wako,"
Yohana alimwambia
Herode. Herode alijua
kuwa maneno haya
yalikuwa kweli. Alijua
kuwa Yohana alikuwa
mtumishi wa Mungu,
mtu mtakatifu.



Lakini hakutaka
kuacha dhambi.
Na Yohana
hakuacha
kuhubiri
kinyume na
dhambi hata
kama alikuwa
gerezani.



Katika sherehe ya kuzaliwa kwake,
Herode alikuwa na sherehe kubwa.
Binti yake Herodia akamchezea densi.
Hii ilimfurahisha Herode sana.
"Nitakupa kitu chochote utakacho,"
akamahidi. "Hata kama ni nusu
ya ufalme wangu."





"Nitaitisha
nini?" binti yule
akafikiria. Mama
yake mwovu
aliyemchukia
Yohana
akamwambia
atakachoitisha!
Ilikuwa ya
kutisha sana!




"Nipe kichwa cha Yohana
Mbatizaji kwa sahani," binti
yule akamwambia Herode.

Alisikia vibaya, lakini
hakuweza kuvunja ahadi
yake. "Kata kichwa cha
Yohana na ulete hapa,"

Herode akaamuru.

Askari wake
wakamtii.



Kwa huzuni marafiki
wa Yohana wakazika
mwili wake, mtu
mjasiri wa Mungu
na mwaminifu.



Mtu atumwa kutoka kwa Mungu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Luka 1, 3, Marko 6

“Kufafanusha maneno yako kwatia nuru.”
Zaburi 119:130





Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

